JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Ikulu ndogo, Mtaa wa Kawajense"
S. L. P. 275,
50101 KATAVI,
BaruaPepe: rbckatavi@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

KATAVI – APRILI, 2022

KATAVI YAFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIRADI 7 YA MAENDELEO

Ndugu Wanahabari,

Kwa mara nyingine tena nawakaribisha sana katika ofisi za **TAKUKURU** Mkoa wa Katavi. Lengo kuu la kukutana kwetu ni kutoa taarifa ya utendaji kazi wa ofisi yetu ya TAKUKURU Mkoa wa Katavi kwa kipindi cha miezi mitatu ambayo ni kuanzia Januari hadi Machi, 2022.

ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022, katika kutekeleza jukumu lake la kuelemisha na kushirikisha umma katika mapambano dhidi ya rushwa, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Katavi imefanya mikutano 10 ya hadhara katika Wilaya za Mpanda, Mlele na Tanganyika Mkoani Katavi, lengo likiwa ni kuwaelimisha wananchi kuhusu wajibu wao wa kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya Rushwa.

Pia tumefanya vipindi viwili (2) vya Redio, kufungua, kuimarisha klabu (22) za wapinga rushwa katika Shule za Msingi na Sekondari na kufanya maonyesho matatu (3).

Katika maadhimisho ya SIKU YA WANAWAKE DUNIANI tarehe 8 Machi 2022, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Katavi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliadhimisha siku hiyo kwa kutoa semina kuhusiana na Rushwa kwenye kongamano lililofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na onyesho moja lililofanywa na wanachama wa klabu ya wapinga Rushwa ya shule ya sekondari Nsimbo.

Katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Mahakama ya mwanzo na kuhitimishwa kwenye Mahakama ya Mkoa, ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Katavi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliadhimisha siku hiyo kwa kutoa semina kuhusiana na Rushwa na maadili kufaya onyesho moja lililofanywa na wanachama wa klabu ya wapinga Rushwa ya shule ya sekondari Nsimbo.

Vilevile, katika utekelezaji wa mpango kazi wa **TAKUSKA** (Mpango wa kufundisha vijana wa skauti kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa), TAKUKURU Mkoa wa Katavi iliweza kutoa semina kwa vijana 31 wa Skauti katika Halmashauri za Nsimbo, Tanganyika na Manispaa ya Mpanda lengo likiwa nikuwajenga vijana katika misingi ya Uzalendo, Uwajibikaji na kutojihusisha na Vitendo vya Rushwa.

UZUIAJI RUSHWA

Ndugu Wanahabari,

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Katavi imefanya kazi ya ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo saba (07),** yenye jumla ya thamani ya shilingi **2,346,844,793/=.** Pia tumefuatilia ujenzi wa Vyumba vya Madarasa ya shule za sekondari na vituo shikizi namba. 5,441, chini ya Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi wa kituo cha afya Nsemlwa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda **shs. 400,000,000/=**;

(ii) Ujenzi wa Daraja la Kashaulili, barabara ya Kashaulili na barabara ya Kamakuka Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda **sh. 431,561,409/=** ;

(iii) Ukarabati wa barabara yenye jumla ya **Km 17.1** ya Njiapanda, Kapemba Getini, Isenga, Ifumbula HQ Road, Mgansa, Ipwaga na Mazwe Halmashauri ya wilaya ya Tanganyika **sh.224,669,850/=;**

(iv) Mradi wa barabara **Km 27.53; Upgrading Kamjela Mnarani-Kusi-Zahanati Busongola Road (Km 23.53), Mgansa-Ipwaga-Mazwe (Km 4) and five(5) lines of cast Insitu Concrete piped culvets** Halmashauri ya wilaya ya Tanganyika **sh. 421,833,300/=**;

(v) **Periodic Maintenance along Ikaka-Kamsanga road 9.35km,Routine Maintenance of Santa Maria-Kabage 8.2 km and construction of 12 lines of culverts** Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika **sh.258,936,550/=;**

(vi) **Spot Improvement along Sibwesa-Katuma road 5.6km and construction of five(5) lines cast in situ concrete pipe culverts** Halmashauri ya wilaya ya Tanganyika **sh.117,835,100/=;**

(vii) Ufunguzi wa barabara ya Tambazi, Msaginya, Kanoge, Kambana River, Katumba HC, Kalungu River Road, Mnyaki, Kabulonge Road, Mtapenda, Ndurumo jumla ya Km 40.1 Halmashauri ya Nsimbo **sh. 470,014,000/=:**

Lengo la ufuatiliaji huu ni kuangalia iwapo kuna mianya ya Rushwa kwenye utekelezaji wa miradi na kuongeza uwazi na upatikanaji wa thamani ya fedha kwenye miradi ya Serikali ili kuboresha huduma kwenye shughuli za

Serikali. Miradi iliyofuatiliwa bado inaendelea kukamilishwa na hakuna mapungufu yaliyobainishwa kwa sasa.

Kama nilivyoeleza, TAKUKURU Mkoa wa Katavi, imefuatilia pia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za sekondari na vituo shikizi namba. 5,441, chini ya Mpango wa Maendeleo na Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19, zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan**. Kupitia mpango huu, mkoa wa Katavi ulipokea jumla ya **sh. 8,580,000,000/=** kama ifuatavyo;

- Halmashauri ya wilaya ya Tanganyika **sh.3, 920,000,000/=** kwa ajili ujenzi wa vyumba **69** vya madarasa shule za sekondari na **127** shule shikizi.
- Halmashauri ya wilaya Nsimbo **sh.1, 740,000,000/=** kwa ajili ujenzi wa vyumba **43** vya madarasa shule za sekondari na **44** shule shikizi.
- Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda **sh.1, 260,000,000/=** kwa ajili ujenzi wa vyumba **48** vya madarasa shule za sekondari na **11** shule shikizi.
- Halmashauri ya wilaya ya Mlele **sh. 680, 000,000/=** kwa ajili ujenzi wa vyumba **24** vya madarasa shule za sekondari na **10** shule shikizi.
- Halmashauri ya Mpimbwe **sh. 980,000,000/=** kwa ajili ujenzi wa vyumba **18** vya madarasa shule za sekondari na **31** shule shikizi.

Katika kusimamia miradi hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Katavi **Mhe. Mwanamvua Hoza Mrindoko** aliunda timu za ufuatiliaji katika Halmashauri hizo**.** Katika ufuatiliaji huo ukiukwaji wa taratibu katika kukamilisha miradi hiyo ulibainika,wizi wa vifaa vya ujenzi, matumizi mabaya ya fedha za mradi, ujenzi kutokamilika kwa wakati, malipo ya mafundi kucheleweshwa na baadhi ya samani (viti na meza) kutengenezwa chini ya kiwango. Baada ya ubainishwaji wa makosa hayo, ofisi ya TAKUKURU ilichukua hatua stahiki ni pamoja na kutoa maelekezo kwa waliotengeneza samani za shule chini ya kiwango, warudie kutengeneza

kwa gharama binafsi na kuhakikisha mafundi waliomaliza kazi zao wanalipwa, pia kuanzisha uchunguzi kwa makosa mengine ya wizi wa vifaa vya ujenzi na matumizi mabaya ya fedha za mradi.

UCHAMBUZI WA MIFUMO

Ndugu Wanahabari,

TAKUKURU mkoa wa Katavi, imefanya Uchambuzi wa mfumo wa madini ujenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika na mfumo wa utendaji kazi wa TEMESA lengo likiwa ni kuangalia mianya ya Rushwa na kutoa Mapendekezo ili kupunguza vitendo vya Rushwa vinavyoweza kujitokeza. Hakuna mapungufu yenye viashiria vya rushwa yaliyobainika katika uchambuzi huo.

UCHUNGUZI

Ndugu Wanahabari,

Katika kipindi cha Januari – Machi, 2022 jumla ya malalamiko **61** yalipokelewa, kati ya hayo malalamiko **57** yalihusu vitendo vya rushwa na malalamiko **4** hayakuhusisha vitendo vya Rushwa. Kutokana na malalamiko 4 ambayo hayakuhusu rushwa, walalamikaji walihitaji ufafanuzi zaidi na walieleweshwa, kushauriwa na wengine walielekezwa mahali sahihi pa kupeleka malalamiko yao hasa Polisi na Mahakamani. Malalamiko 57 ambayo yalihusu rushwa yalifunguliwa majalada ya uchunguzi ambapo majalada mawili (02) - uchunguzi wake ulikamilika na kufikisha watuhumiwa mahakamani. Majalada 55 bado yanaendelea na uchunguzi.

Mchanganuo wa malalamiko **61** yaliyopokelewa kwa kipindi hicho ni kama ifuatavyo-:

SN	IDARA/SEKTA	IDADI
1	AMCOS	1
2	Ujenzi	2

3	Polisi	1
4	Elimu	7
5	Mahakama	1
6	Maliasili	2
7	Afya	12
8	Mazingira	1
9	TAMISEMI	7
10	Ardhi	5
11	Maji	1
12	Halmashauri	11
13	TANESCO	2
14	Siasa	1
15	Utawala	4
16	TFS	1
17	Hifadhi za Misitu	1
18	Bima	1
	JUMLA	**61**

Katika kipindi husika, **kesi mpya 2** zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya **kesi 11 zilizoendelea mahakamani**. Kesi moja (01) iliamuliwa, ambapo mshitakiwa alipatikana na hatia na kesi kumi (10) bado zinaendelea Mahakamani katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

MIKAKATI KWA KIPINDI CHA JANUARI – MACHI 2022

Ndugu Wanahabari,

Katika kipindi cha Aprili – Juni, 2022, TAKUKURU Mkoa wa Katavi tunatarajia kuongeza nguvu katika uchunguzi wa malalamiko yanayopokelewa hasa yanayohusu ubadhirifu wa fedha za **Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19** zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Samia Suluhu Hassan** katika Halmashauri zote na kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya wajibu wa kila mwananchi kushiriki katika Kupambana

na Rushwa na kutoa taarifa zinazohusiana na vitendo vya Rushwa kwa TAKUKURU.

Kwa upande wa Uchambuzi wa mifumo, TAKUKURU Mkoa wa Katavi itafanya Uchambuzi wa mfumo wa miradi ya barabara inayosimamiwa na TARURA na kuendelea na Uchambuzi wa mfumo wa utendaji kazi wa TEMESA.

Vilevile, kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2022, TAKUKURU Mkoa wa Katavi itafanya uelimishaji wa jamii hususan kupitia ushirikiano kati ya TAKUKURU na Chama cha Skauti nchini – TAKUSKA unaolenga kuwafikia vijana wengi zaidi katika mkoa wetu.

WITO:

Ndugu Wanahabari,

Mwisho natoa shukurani kwenu Wanahabari kwa ushirikiano wenu mkubwa katika Mapambano dhidi ya Rushwa. Aidha, TAKUKURU Mkoa wa Katavi inatoa wito kwa jamii ya wana-Katavi kwa ujumla kutokujihusisha na vitendo vya kijinai kama kuomba na kupokea rushwa za aina zozote zile.

Hivyo tunatoa rai kwa wananchi wote wa Mkoa wa Katavi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kupiga simu ya bure 113 na *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 au kupiga simu ya Mkuu wa TAKUKURU Mkoa ambayo ni **0738-150096** au kufika katika ofisi za TAKUKURU iliyo karibu nawe.

Pia bado kumeendelea kuwa na wimbi la matapeli wanaojifanya ni maafisa wa TAKUKURU ambao hupiga simu kwa watu mbalimbali wakitoa maelekezo na maagizo kwa watu hao ikiwa ni pamoja na kutakiwa kuripoti ofisi fulani ya TAKUKURU au kutaka kuonana na wahusika.

Tunatoa wito na rai kwa jamii na watumishi wote ambao ikitokea wamepigiwa simu na matapeli hao basi wajiridhishe na ofisi ya TAKUKURU iliyoko karibu na maeneo yao au kupiga simu ya bure 113 na *113# au

kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia namba 113 na simu rasmi za TAKUKURU Mkoa wa Katavi ambazo ni 0738150096, 0738150098 (Mlele) na 0738150099 (Tanganyika). Usikubali kutapeliwa, toa taarifa TAKUKURU ili mhalifu huyo aweze kuchukuliwa hatua za kisheria kwani ni kosa la kisheria kujifanya wa TAKUKURU.

Kwa pamoja tushirikiane kuitokomeza rushwa

TANZANIA BILA RUSHWA INAWEZEKANA NA KAZI IENDELEE

Imetolewana:

Festo Mdede
MKUU WA TAKUKURU (M)
KATAVI.
0738-150096